## 6.0 MUDA WA KUFUNGUA SHAURI LINALO HUSU MKATABA

Muda wa kufungua shauri kwa mtu aliyevunja mkataba ni miaka sita. Muda huu huanza kuhesabiwa kuanzia mkataba unapovunjika. Hata hivyo, endapo mtu atashindwa kufungua shauri ndani ya muda ulioanishwa anaweza kuomba kuongezewa muda kwa Waziri wa Katiba na Sheria ambaye kwa kushauriana na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, atatoa amri ya kuongezwa muda kwa ajili ya kufungua shauri husika. Muda utakaoongezwa hautazidi muda wa ukomo wa kufungua shauri ulioanishwa.

## 7.0 HITIMISHO

Ni vizuri kutambua kuwa japokuwa sheria inatambua aina mbili za mkataba wa mdomo na maandishi hatahivyi mktaba wa maandishi ni rahisi kuuthibitisha mahakamani ikiwa utekelezaji wa masharti ya mkataba utakapokumbwa na migogoro.
Vilevile ni vizuri pande za mkataba kuelewa kwa ufasaha masharti ya mkataba wanaoingia kabla ya kuingia mktaba huo ili kufanya maamuzi ambayo hayataleta hasara kwa husika pale sheria itakapochukua mkondo wake.


**Kwa Maoni, wasiliana na Tume kupitia anuani ifuatayo :**

**Katibu Mtendaji,**
**Tume ya kurekebisha Sheria Tanzania ,**

**Jengo la Taaluma Na. 1,**
**Barabara ya Mkalama**
**S.L. P 1718**
**DODOMA**
**TANZANIA**

**Barua pepe: lrct@lrct.go.tz**
**Tovuti: www.rlct.go.tz**


**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

# TUME YA KUREKEBISHA SHERIA TANZANIA

# MASUALA MUHIMU YA KUZINGATIA KATIKA MIKATABA



## 1.0 UTANGULIZI

Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania (Tume) ilianzishwa mwaka 1980 kwa Sheria ya Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania, Sura ya 171. Kwa mujibu wa Sheria hii pamoja na majukumu mengine, Tume ina majukumu ya kupitia na kutathmini utekelezaji wa sheria zote za Jamhuri ya Muungano kwa lengo la kuziwezesha sheria hizo kuendana na mabadiliko yanayotokea katika nyanja za kijamii, kisiasa, kiuchumi, kisayansi na teknolojia. Aidha, Tume ina jukumu la kutoa elimu ya sheria kwa umma.

## 2.0 MAANA YA MKATABA

Mkataba ni makubaliano yenye nguvu ya kisheria baina ya pande mbili au zaidi yanayofanyika kwa mdomo au maandishi. Makubaliano haya huanisha haki na wajibu wa kila upande katika utekelezaji wa suala linalohusiana na maudhui ya mkataba. Sheria ya Mikataba, Sura ya 345 ndio sheria inayosimamia masuala ya mikataba. Mkataba unaweza kuwa wa mauziano ya ardhi, gari, kupanga nyumba au kuchukua mkopo nk.

## 3.0 SIFA ZA MKATABA

Makubaliano yote si lazima yawe ni mkataba. Ili makubaliano yawe mkataba ni lazima pande husika katika

mkataba zizingatie vigezo maalum kabla ya kuingia katika mkataba. Vigezo hivyo ni;

### 3.1 Ridhaa

Pande zinazoingia katika mkataba zinatakiwa kuingia katika mkataba kwa hiyari yao bila kushawishiwa, kulazimishwa, kulaghaiwa, kuhadaiwa, kushurutishwa au kudanganywa kwa namna yoyote ile.

### 3.2Malipo Halali

Mkataba wowote unapaswa kuwa na malipo halali kisheria. Malipo yanaweza kuwa fedha, mali au kitu chochote.

### 3.3 Lengo la Makubaliano liwe linakubalika kisheria

Pande husika katika mkataba zinapaswa kuingia katika makubaliano yanayohusu jambo ambalo linaruhusiwa kisheria. Mathalan, hairuhusiwi kuingia katika mkataba kwa ajili ya kutekeleza uhalifu au kuuziana mali iliyopatikana kwa njia ya wizi.

### 3.4 Uwezo wa Kuingia Katika Mkataba

Ili makubaliano yawe na nguvu ya kisheria ni lazima yawe yameingiwa na pande ambazo zina uwezo kisheria kuingia katika mkataba. Kimsingi mkataba inabidi uingiwe na:-

- mtu ambaye ana akili timamu na
- umri wa kuanzia miaka 18. Mtu aliye na umri wa chini ya miaka 18 anaruhusiwa kuingia mkataba ambao unahusu mahitaji muhimu tu si vinginevyo.
- Aidha, ikiwa upande husika ni kampuni mtu anayeingia mkataba ni lazima awe mtu ambaye amepewa mamlaka ya kufanya hivyo na kampuni husika.

## 4.0 UVUNJAJI WA MKATABA

Kuvunja mkataba ni hali ya kutotimiza makubaliano/wajibu ulioanishwa katika mkataba. Mkataba unaweza kuvunjika katika mazingira yafuatayo;

- Kukiuka masharti yaliyoanishwa katika mkataba au kushindwa kuyatekeleza.
- Kumaliza kutekeleza wajibu wao kwa mujibu wa mkataba
- Pande zilizoingia mkataba kukubaliana kwa pamoja kuvunja mkataba
- Mkataba kuvunjika kwa sababu ya kujitokeza kwa masuala ambayo yapo nje ya uwezo wa wahusika na na hayakutarajiwa kama vile jambo mlilokubaliana kulitekeleza katika mkataba limeharikiba, kifo, mabadiliko ya sheria ambayo yanafanya mkataba usiwe halali, kifo, vita n.k

## 5.0 NAFUU

Baada ya mkataba kuvunjika, upande wowote ambao unaona haki zake zimekiukwa unaweza kufungua shauri mahakamani ili kudai haki hizo. Baada ya Mahakama kudhibitisha ukiukwaji huo inaweza kutoa nafuu zifuatazo;

- Kulipwa fidia kutokana na madhara yaliyosababishwa na kuvunjika kwa mkataba.
- Kutekeleza masharti ya mkataba kama ilivyokubaliwa katika mkataba.
- Kuomba zuio la muda wakati shauri linaendelea ili kuzuia madhara yatokanayo na mkataba kutokutekelezwa.
- Upande ambao haukukiuka masharti ya mkataba kubatilisha mkataba bila kudai fidia.